BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 02 Machi, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Bajeti ya Ziada (Supplementary Budget) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Bajeti ya ziada (Supplementary Budget) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

Mjumbe wa Kamati ya Wabunge Watano Wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

Ripoti ya Wajumbe watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

150. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Jiji la Zanzibar hivi sasa limekuwa na shughuli nyingi za kimaendeleo pamoja na ongezeko la vyombo vya usafiri kama vile piki piki, bajaji na gari, kumbi za burudani na kumbi za shughuli za kijamii. Hali hii inasababisha uchafuzi mkubwa wa hali ya hewa (noise pollution) kutokana na kelele za vyombo na sauti za juu za muziki kwenye kumbi hizo.

(a) Kwa kuwa hali hiyo siyo nzuri kiafya, je, Serikali inachukua hatua gani kuidhibiti.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuzuia usafiri wa piki piki maeneo ya Mjini ili kuondoa kelele (noise pollution) hizo.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuweka masharti kwa kumbi zinazofanyika shughuli za kijamii kuwekwa miundombinu ya kudhibiti sauti (sound proof) ili kudhibiti kelele zinazowakera wananchi.

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

96. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Ni muda mrefu sasa wananchi wa Kimbuni, shehia ya Mgagadu wanasubiria kisima cha umwagiliaji, huku wakiendelea kusubiria ahadi zilizotolewa kuwa kisima hicho kitakabidhiwa kwao.

Je, ni lini wananchi hao watapatiwa kisima hicho.

### Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

129. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa nchi yetu inafungamana na mabadiliko ya kidiplomasia inayoendana na Diplomasia ya Uchumi.

(a) Je, kwa kiasi gani Diplomasia ya Uchumi inachangia katika kuleta mageuzi kwenye falsafa ya Uchumi wa

Buluu.

(b) Je, vipi balozi zetu katika mataifa mbali mbali rafiki zinayahamasisha mataifa yaliyobobea kwenye Uchumi wa Buluu kuisaidia Zanzibar kupiga hatua kubwa kwenye sekta hii.

(c) Ni mafanikio na changamoto zipi zinazozikumba balozi zetu katika mikakati yao ya kuimarisha na kuukuza Uchumi wa Buluu.

<u>Wizara ya Afya:</u>

52. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na jitihada za Serikali, vifo vya watoto na vifo vya uzazi vya mama vimekuwa tishio Zanzibar. Aidha, suala la lishe bora limekuwa kikwazo katika kuhakikisha afya ya watoto inakuwa bora, hasa kwa watoto wanaotoka kaya masikini ambazo hazikubahatika kukubaliwa na TASAF.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba kila mtoto anapewa lishe bora kwa ajili ya ukuwaji na kupata kinga bora ya mwili.

(b) Je, ni upi mpango bora wa Serikali wa kuongeza wataalamu wa kutosha na kwa uwiano ili kupunguza vifo vya watoto wakati wa kuzaliwa, hasa katika vituo ambavyo ‘Orderly’ wanahusika na kuzalisha.

167. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwepo na ukosefu wa madaktari katika siku za Jumamosi na Jumapili pamoja na siku za Sikukuu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Jambo ambalo ni hatari kwani kunatokezea wagonjwa wa dharura kama vile majeruhi wa ajali na maradhi mengine ya ghafla.

Je, Serikali imejipangaje katika kuwalipa madaktari posho za kufanya kazi siku za mapumziko, ili waendelee kuwahudumia wananchi kama vile siku nyengine za kazi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

136. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kituo cha Habari na Elimu kinachomilikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kilichopo katika skuli ya sekondari ya Kwarara, kina mchango mkubwa katika kuisadia Wizara kupitia utoaji wa taarifa na maendeleo kupitia TEHAMA.

(a) Je, Wizara haioni umuhimu wa kukiboresha kituo hiki kwa kukipatia huduma na vitendea kazi ili kiende sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia.

(b) Kwa kuwa radio ya elimu FM imebuni vipindi vizuri, je Wizara haioni kwamba ipo haja ya kuwaajiri vijana kwa mujibu wa taaluma za elimu zenye mnasaba na tasnia ya habari.

(c) Televisheni ya kituo hiki inayopatikana kwenye king'amuzi cha ZMUX bado haijapata wataalamu husika kwa tasnia ya habari, Je Wizara ina mkakati gani wa kufanya maboresho ya EZ TV.

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kusoma vitabu ni moja ya njia ya kujiongezea ujuzi na maarifa makubwa.

(a) Ni kwa kiasi gani mabadiliko tunayoyatarajia katika sekta ya elimu kwa upande wa mitaala imelitupia jicho wazo la kuwawezesha vijana wetu tabia ya kujisomea vitabu.

(b) Je, vipi Maktaba ya Taifa ya Zanzibar inawahamasisha wananchi kufika kwa wingi na kuweza kuchota bahari ya elimu kupitia tasnia hii ya kusoma vitabu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

123. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Zanzibar ina historia kubwa sana katika sekta ya michezo na sanaa, lakini bado wanamichezo na wasanii wa Zanzibar hawanufaiki ipasavyo na vipaji vyao.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wanamichezo na wasanii wa Zanzibar, ili wanufaike kimaisha kupitia vipaji vyao.

146. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kamati ya Mapinduzi Cup, kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inastahili pongezi kwa kuyaendeleza mashindano ya Mapinduzi Cup kwa nia ya kuyaenzi Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Hata hivyo, kuna baadhi ya michezo kama vile mpira wa kikapu, mpira wa mikono na skwashi ambayo haionekani kupewa kipaumbele kama ilivyo kwa mpira wa miguu, wakati vyama vyao vya michezo kushiriki sherehe za Mapinduzi.

(a) Je, Wizara inafahamu kuwepo kwa michezo inayofanywa na vyama hivyo wakati wa sherehe za Mapinduzi.

(b) Je, Wizara inashirikiana vipi na vyama hivyo katika maandalizi, matangazo na kuhamasisha ushiriki wa vyama hivyo kwenye sherehe za Mapinduzi.

(c) Je, Wizara ina mpango gani wa kuyaweka mashindano yanayoandaliwa na vyama hivyo vya michezo kwenye kalenda ya sherehe za Mapinduzi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

83. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na juhudi za Serikali za kuwatengenezea mazingira mazuri wasafiri wanaotumia vyombo vya usafiri baharini, kwa kuwajengea na kuwawekea viti abiria hao, kumejitokeza tatizo la muda mrefu la viti vinavyokaliwa na abiria kuharibika kiasi ya kuwa ni hatari kwa miili yao na hata kuwachania nguo zao.

Je, kuna utaratibu gani wa kuvibadilisha viti hivyo.

104. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna safari za Pemba-Tanga kila siku ya Jumapili na kurejea siku ya Jumatatu. Kupitia safari hizo, kuna usumbufu mkubwa kwa abiria kutokana na kutokuwepo kwa muda mahsusi wa kuondoka meli hizo.

(a) Kwa nini usipangwe muda muafaka wa safari hizi wa kuondoka kwa meli husika.

(b) Kwa nini meli hizo zinajiondokea tu muda wanaotaka wao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Mti wa mlangilangi ni moja kati ya miti maarufu inayopotea nchini kwetu.

(a) Je, kuna faida gani za kiuchumi, kiafya na kiutamaduni zinazotokana na mti huu.

(b) Je, Wizara yako ina mkakati gani wa kuwawezesha wananchi kunufaika na zao la mti huu ili waweze kujipatia kipato.

(c) Je, ni kwa kiwango gani mti wa mlangilangi unapotea visiwani Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni maeneo gani Zanzibar yanayoongoza kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii.

(b) Ni maeneo gani yanayoongoza kwa kutembelewa na watalii wengi zaidi.

(c) Je, utalii wa ndani unachangia asilimia ngapi ya pato la taifa kwa sasa.

IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taarifa ya Serikali Kuhusu Bajeti ya Ziada (Supplementary Budget) kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya ujenzi wa soko la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini.

V. RIPOTI YA WAJUMBE WATANO WANAOLIWAKILISHA BARAZA LA WAWAKILISHI KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:

Mjumbe wa Kamati ya Wabunge watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

Ripoti ya Wajumbe watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
02 Machi, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.